# KAS: udini utaondoa amani ya Tanzania

ELIAS MHEGERA

MKURUGENZI Mkazi wa Shirika la Kijerumani la Konrad Adenauer Stiftung (KAS), Stefan Reith amewataka Watanzania kuienzi amani iliyopo na kuonya kwamba mambo ya udini yanayoendelea sasa nchini yanaweza kusababisha amani kutoweka.

Akiongea ofisini kwake mtaa wa Isimani Upanga hivi karibuni muda mfupi kabla hajaelekea Arusha kikazi, aliwaasa Watanzania kwamba mwaka huu wa 2013, uwe ni wa amani na kuachana na mivutano isiyo na tija.

"Amani na utulivu ni mahitaji muhimu popote duniani ili kuleta maendealo ya nchi, naamini wananchi wengi wa nchi hii wanalifahamu vyema jambo hili kutokana na historia iliyokuwapo kwa muda mrefu," anasema.

Angalizo hilo la Reith linakuja huku Watanzania wakiwa bado wanakumbukumbu za matukio ya aina yake ya uchomaji wa makanisa yaliyotokea Zanzibar na Mbagala jijini Dar es Salaam.


Lakini, akizungumzia zaidi umuhimu huo wa amani anasema kwa kuzingatia hilo ndiyo maana shirika lake limedhamini mikutano kadhaa iliyowakutanisha Waislam na Wakristo mara kadhaa mwaka jana.

Anasema lengo la mikutano yote hiyo ilikuwa ni kupunguza




Juu: Mkurugenzi Mkazi wa KAS, Stefan Reith

"Baada ya kuona tofauti za dini zikiachwa zien-delee zinaweza kuleta



Anasema lengo la mikutano yote hiyo lilikuwa ni kupunguza nyufa za udini miongoni mwa watu wenye dini tofauti.

Hoja za Reith ziliungwa mkono na maafisa waandamizi katika ofisi hizo za KAS ambao ni Richard Shaba na Erasto Ndeuka.

Wakichangia kwa nyakati tofauti wote wanasema kimsingi Watanznania bado ni watu wanaopendana isipokuwa kuna watu wachache wenye ajenda zao za siri wanaochochea migogoro ya udini.

Wanaurejea mkutano wa siku mbili tarehe 28 na 29 Novemba mwaka jana, uliofanyika pale New Africa Hotel ambapo viongozi hao wa kiroho walionyesha kwamba wanapenda tofauti zilizopo zijadiliwe kiungwana zaidi badala ya kutanguliza jazba.

"Baada ya kuona tofauti za dini zikiachwa ziendelee zinaweza kuleta madhara makubwa tuliamua kuwakutanisha watumishi wa Mungu na hatukutaka vyombo vya habari viripoti mjadala huo ili watu waliokuwapo katika mjadala huo wawe na uhuru zaidi," anasema Shaba.

Alikuwa anazungumzia mkutano ambao ni mmoja kati ya mingi ambayo shirika la KAS na Baraza la Madhehebu kwa Amani Tanzania (IRCPT), yamekuwa yakiandaa kwa pamoja kwa lengo la kuleta amani na kujadiliana mambo kadhaa ya kimaendeleo.

Kwa upande wake afisa mwandamizi katika shirika hilo Ndeuka anasema kabla ya kuitisha mkutano huo ilibidi kwanza wakusanye taarifa mbali mbali zinazoizunguka migogoro ya udini na kisha kuwaomba watumishi hao na wao watoe msimamo wao.

**"...za dini zikiachwa ziendelee zinaweza kuleta madhara makubwa tuliamua kuwakutanisha watumishi wa Mungu na hatukutaka vyombo vya habari viripoti mjadala huo ili watu waliokuwapo katika mjadala huo wawe na uhuru zaidi**

Miongoni mwa viongozi waliohudhuria katika mjadala huo walikuwa ni kutoka madhehebu mbali mbali ya Kikristu, Waislam, Baahai, na Wahindu.

Kwa upande wao akina mama na vijana waliamua kwamba watazidisha mikutano ya aina hiyo ili ifanyike mara kwa mara.

Tayari vijana wanao umoja wao uitwao Amani Group, ambao lengo lake kuu ni kuwakutanisha ili kujadiliana masuala kadhaa ya kimaendeleo.

Katika kukemea matatizo ya udini mwenyekiti wa BAKWATA tawi la wanawake mama Shamim Khan anasema lipo tatizo la baadhi ya watu kusoma maneno ya vitabu vitakatifu kwa ufupi tu na kabla hawajaelewa vizuri hukurupuka kwenda kushambulia dini za watu wengine.

Mama Khan ambaye alipata kuwa naibu waziri katika serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, alikuwa akiongea katika moja ya mikutano iliyoandaliwa na KAS kwa kushirikiana na shirika lingine la kiraia TADIP-Maendeleo katika mkutano uliofanyika hoteli ya Serena mwishoni mwa mwaka jana.

Shirika la KAS linajivunia mashirikiano yake na taasisi mbali ambazo zimelenga kuwaendeleza

Stefan Reith

**Picha za kulia:** Kiongozi wa Kanisa Katoliki nchini Tanzania Muadhama Polycarp Kardinali Pengo na Kiongozi wa Waislam Sheikh-Muft Issa Bin Shaaban Simba





Watanzania kupitia nyanja mbali mbali kama ilivyokuwa kwa Jumuiya ya Waalimu Wanaosomesha Qur'ani Tanzania (JUWAQUTA) ambao mwaka jana pia walifanya mikutano kadhaa iliyoandaliwa kwa pamoja kati yao na shirika hilo kutoka ujerumani.

Jitihada hizo pia ziliwakutanisha vijana wa madhehebu tofauti katika umoja wao unaoitwa JUVIWAWA ambapo walikutana katika hoteli ya Protea kwa siku nzima wakijadiliana juu ya mustakabali wao na jinsi ambavyo dini zao zinaweza kutumika kama chachu ya maendeleo.

Wakati jitihada zote hizo zikiendelea bado yapo matukio ya hapa na pale kama ilivoripotiwa katika vyombo vya habari ambapo Waislamu na Wakristu wamejikuta katika mivutano ya hapa na pale. .

Mifano ya hivi karibuni kabisa ni ya mkoani Mwanza na katika mkoa mpya wa Geita katika mji wa Katoro ambapo polisi waliingilia kati kuzuia mgogoro unaohusu nani achinje na nani asichinje wanyama kwa ajili ya kitoweo.

Mgogoro kama huyo ulileta sokomoko mara baada ya Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Evaristi Ndikilo kusema kwamba, wanaotambuliwa kisheria kwamba wanastahili kuchinja wanyama wa kitoweo ni Waislam jambo ambalo lilisabisha mjadala mkali hata katika vyombo vya habari.

Na labda kituko cha hivi karibuni kabisa kilihusu baadhi ya watu waliotajwa kama Waislamu "wenye hasira kali" kuvamia shule moja huko Bahi mkoani Dodoma na kuyatoboa masufuria ya shule kwa kile kilichodaiwa kwamba masufuria hayo yalitumika katika kuchemsha maji kwa ajili ya kuchuna ngozi ya nguruwe.

Pamoja na mijadala hii mizuri yaelekea bado kuna maduku duku ambayo hayajapatiwa ufumbuzi na hivyo jusababisha mivutano ya mara kwa mara.

Yakiwamo Mahakama za Kiislamu za Kadhi, kujiunga kwa Tanzania na Jumuia ya Nchi za Kiislamu za OIC na pia Ijumaa kufanywa siku ya mapumziko kama ilivyo kwa Jumamosi na Jumapili.

Ipo pia hoja kwamba Wakristu wmeshika nafasu nyingi za madaraka kuliko Waislamu hayp ni miongoni tu mwa mambo ambayo yataendelea kusababisha mivutano hiyo.